



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA ITILIMA



Unapojibu taafadhali taja:
Kumb. Na. AG.22/124/04/58

Tarehe:27/01/2021

TANGAZO LA NAFASI ZA YA MWENYEKITI WA BODI YA AJIRA

Kwa mujibu wa Matakwa ya Kanuni ya 127 ya kanuni za Utumishi wa Umma,2003 Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Itilima anakaribisha maombi ya watanzania wote wenye sifa za kujaza nafasi ya Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira ya Halmashauri ya Wilaya ya Itilima.

1. MWENYEKITI WA BODI YA AJIRA– NAFASI 1

1.1 SIFA ZA MWOMBAJI

- i. Awe Mtanzania
- ii. Awe na taaluma ya Sheria,Rasilimali watu au Utawala.
- iii. Awe ni mtumishi wa Umma aliyestaafu.
- iv. Awe ni mkazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Itilima.

1.2 MAJUKUMU

- i. Kuendesha vikao vya Bodi ya Ajira kwa Mujibu wa Kalenda za Vikao vya Halmashauri ya Wilaya ya Itilima
- ii. Kufanya usaili kwa kada zinazofanyiwa usaili na Halmashauri ya Wilaya kwa kuzingatia Sheria ,Kanuni na Taratibu katika Utumishi wa Umma,
- iii. kupitisha mapendekezo ya kuthibitisha watumishi kazini,kupandisha vyeo na kuwabadilishia vyeo watumishi kwa mujibu wa Sheria ,Kanuni na Taratibu katika Utumishi wa Umma.
- iv. Kumshauri mwajiri kuhusu masuala ya Ajira, kuthibitisha kazini watumishi,upandishwaji vyeo au kubadilishwa vyeo kwa watumishi kwa kuzingatia Sheria ,Kanuni na Taratibu katika Utumishi wa Umma.

Halmashauri ya Wilaya ya Itilima, S. L. P 308, Itilima, Simu +255 028 2986329, Barua pepe:
info@itilimadc.go.tz Tovuti: www.itilimadc.go.tz

2 MASHARTI YA JUMLA

- i. Waombaji wote wapitishie barua zao kwa Mtendaji wa Kijiji/Mtendaji Kata katika eneo analoishi.
- ii. Mwombaji awasilishe picha moja ya hivi karibuni.
- iii. Vyeti vya taaluma.
- iv. Maelezo Binafsi (CV)
- v. Barua ya kustaafu katika utumishi wa Umma.
- vi. Kazi hii ni ya muda, kwa muda wa miaka mitano.
- vii. Kazi hii haina mshahara, malipo ni posho ambayo inategemea uhudhuriaji wa vikao vya Bodi ya Ajira.
- viii. **Mwisho wa kupokea maombi haya ni tarehe 09/02/2021 saa 9:30 Alasiri.**
- ix. **Maombi yasiyozingatia vigezo vilivyoainishwa hayatashughulikiwa.**

MUHIMU: Kumbuka kuambatanisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vielelezo vyote vilivyotakiwa. Maombi yote yatumwe Kwa:-Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya S.L.P 308 .ITILIMA.



Elizabeth M Gumbo
**MKURUGENZI WA MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
ITILIMA**

MKURUGENZI MTEINDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
ITILIMA